BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA TISA

Kikao cha Tano – Tarehe 12 Mei, 2025

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2025/2026.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC):**

Hotuba ya maoni ya Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali (PAC) kuhusu Hotuba ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora (Bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) kwa Mwaka 2025/2026.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

213. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Tathmini iko vipi juu ya uelewa wa wananchi katika suala zima la kukuza Haki za Binadamu nchini.

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

105. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Uhaba wa vifaa kwa kiasi kikubwa unakwamisha zoezi la uchukuaji wa taka katika maeneo mbali mbali ya mji wa Zanzibar.

Ni yepi matarajio ya Serikali katika kupambana na changamoto hii.

### Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

95. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:

Ni vikwazo vipi vinavyowakabili wanawake katika harakati zao za maisha kwa ujumla hivi sasa.

### Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

200. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

(a) Sera ya biashara inazungumzia vipi juu ya suala zima la usalama wa chakula.

(b) Tathmini ya uelewa wa wananchi iko vipi juu ya swala hili kwa ujumla wake.

**Wizara ya Maji na Nishati:**

238. MHESHIMIWA DKT. SOUD NAHODA HASSAN (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini.

Katika ujenzi wa barabara ya Kitogani hadi Paje kumejitokeza changamoto ya uharibifu wa miundombinu ya maji katika shehia ya Kitogani.

(a) Je, ufahamu wa Wizara yako ukoje juu ya tatizo hili.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuwarudishia wananchi huduma hiyo.

(c) Je, kuna mashirikiano gani ya Taasisi za Serikali kabla ya ujenzi wa barabara kuanza ili kunusuru gharama za ziada kwa Serikali.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

237. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Katika shehia ya Mtangani kuna mbuyu unaojulikana kwa jina la Vasco Dagama ambae inasemekana alitembelea katika kijiji hicho tarehe 6/4/1498 akiwa na ujumbe wa watu 84 na akiwa na vyombo vitatu vya kusafiria kwa wakati huo.

(a) Ni vipi Wizara yako inaitambua historia hii.

(b) Je, huyu Vasco Dagama alitokea nchi gani na alikuwa na madhumuni gani yaliyomfanya atembelee shehia ya Mtangani.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**12 Mei, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA**